



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Nane – Tarehe 24 Mei, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2024/2025.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Mwaka 2024/2025.

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

169. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Hivi karibuni kumeibuka mitandao mbali mbali ya fedha mtandao hapa Zanzibar, ikiwemo Safeland na Fabric Africa.

- (a) Je, ni mitandao gani halali ambayo wananchi wanaweza wakawekeza fedha zao kwa usalama kwa kuwa ulimwengu unakwenda kwenye mfumo wa kimtandao.
- (b) Ni mitandao ipi ya kifedha ambayo Serikali haiitambui na Je, Serikali imewahi kuwatahadharisha wananchi kuwacha kuwekeza fedha zao huko.
- (c) Je, Serikali ina taarifa ya wizi na udanganyifu wowote unaofanywa na baadhi ya mitandao hiyo kwa kuwaibia wananchi fedha zao.

Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

215. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Ni mikakati gani Wizara yako inaichukua katika kupunguza changamoto za wawekezaji kutoka mataifa mbali mbali duniani.

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

112. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Baadhi ya nchi ikiwemo Tanzania kupitia taasisi za viwango kama vile Tanzania Bureau of Standards (TBS), zimechukua hatua ya kupiga marufuku uingizaji wa bidhaa za kucha na kope bandia pamoja na vipodozi 12 vyenye kemikali hatari nchini, baada ya tafiti kuonyesha madhara makubwa kwa watumiaji wa bidhaa hizo, hasa kwa wanawake wanaozitumia.

- (a) Je, Serikali inalitambua tatizo hili, na imechukua hatua gani kupunguza athari hizi kwa jamii yetu.
- (b) Je, kuna mikakati gani maalum inayotekelezwa na Serikali ili kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya bidhaa hizi.
- (c) Je, Serikali ina mfumo upi wa udhibiti wa usalama na ubora wa bidhaa zinazolingizwa nchini, na ni hatua gani zinazochukuliwa ili kuhakikisha bidhaa zote zinazopatikana sokoni zinafaa kwa matumizi na hazileti madhara.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

47. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:
- (a) Je, kuna utafiti wowote uliofanywa kuhusiana na kuku aina ya peduu (paja nono) juu ya usalama wa afya ya mtumiaji na kujiridhisha kuwa hawana athari yoyote kwa mlaji.
 - (b) Kwa kiasi gani uingizwaji wa kuku aina ya peduu kutoka nje unaathiri soko la ndani ya Zanzibar.
 - (c) Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuinua wafugaji wetu wa ndani.

Wizara ya Maji, Nishati na Madini

259. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na Wizara yako, bado ipo tabia ya baadhi ya wananchi wanaopinga maendeleo kwa kuiba maliasili zisizorejesheka na kuzitumia bila ya kufuata utaratibu wa kisheria.

- (a) Je, Wizara yako inalishughulikia vipi tatizo hilo.
- (b) Watu wangapi wamewahi kukamatwa na kutiwa hatiani kwa makosa haya.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

82. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa na mpango wa kujenga viwanja vya ndege ndogo ndogo katika vijiji vya Nungwi, Mwambe na Paje. Tunaishukuru Serikali kwa kujenga kiwanja cha ndege hapo Nungwi, ingawa bado haijajenga kiwanja chengine mpaka sasa katika kijiji cha Mwambe wala Paje.

- (a) Je, bado Serikali inalo lengo la kujenga viwanja hivyo.
- (b) Je, unawaeleza nini wananchi wa Zanzibar juu ya suala hili.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

180. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tafiti zinaonesha kwamba ufaulu mdogo kwa wanafunzi wa Kidato cha Nne na Sita unasababishwa na wanafunzi hao kushindwa kumudu lugha ya Kiingereza.

- (a) Je, Wizara yako imebaini nini kuhusiana na chanzo cha changamoto hii.
- (b) Nini kifanyike ili kuhakikisha tatizo hili linaondoka nchini.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2024/2025.

Zanzibar,
24 Mei, 2024.


(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA